**HOTUBA YA IJUMAA**

**المعاصر واقعنا في الأولويات وفقه الأواخر العشر**

kumi la mwisho na fiqhi ya vipaombele ndani ya wakati wetu wa sasa.

Imefasiriwa

na

profesa Ayman Alasar

Namshukuru Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe. Msemaji ndani ya Kitabu chake Kitukufu: **سَابِقُوا إِلَى مَغْفِرَةٍ مِنْ رَبِّكُمْ وَجَنَّةٍ عَرْضُهَا كَعَرْضِ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ أُعِدَّتْ لِلَّذِينَ آمَنُوا بِاللَّهِ وَرُسُلِهِ** {**kimbilieni msamaha wa Mola wenu na Pepo upana wake ni kama upana wa mbingu na Ardhi imeandaliwa kwa ajili ya wale walioamini Mwenyezi Mungu Mitume yake**}. Ninashuhudia kuwa hakuna mola wa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika, na ninashuhudia kuwa Mtume Muhammad ni mja wake na Mtume wake. Ewe Mwenyezi Mungu peleka rehma amani na baraka kwake na kwa watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake na wale wote waliowafuata kwa wema mpaka siku ya mwisho.

**Baada ya utangulizi**:

Miongoni mwa rehma za Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa waja wake ni pamoja na kulifanya kumi la mwisho la Mwezi wa Ramadhani kuwa ni msimu wa ongezeko la malipo mema na kukimbilia kufanya mambo ya kheiri, ambapo nafsi huchangamke wakati wa kukaribia mwisho, kwani Mtume wetu SAW alikuwa anatumia vyema nyakati bora, ambapo Bibi Aisha R.A anasema: Mtume SAW alikuwa anafanya jitihada za ibada ndani ya kumi la mwisho zaidi ya wakati mwengine wowote, na anasema R.A: Mtume S.A.W pindi linapoingia kumi la mwisho alikuwa akihuisha usiku na kuamsha watu wa nyumbani kwake na kufunga mkanda.

Miongoni mwa mambo ya kumfuata Mtume SAW ni pamoja na kuhuhisha usiku wa kumi la mwisho la mwezi wa Ramadhani kwa kuswali kusoma Quran kuleta dhikri istighfari na kutoa katika mambo ya kheir, kwani huu ndio mwenendo wa

waja wema na ni ibada za wacha-Mungu, ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema katika wasifu wa watu wa Peponi:

**تَتَجَافَى جُنُوبُهُمْ عَنِ الْمَضَاجِعِ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ خَوْفًا وَطَمَعًا وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنْفِقُونَ * فَلَا تَعْلَمُ نَفْسٌ مَا أُخْفِيَ لَهُمْ مِنْ قُرَّةِ أَعْيُنٍ جَزَاءً بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ.**

{**Mbavu zao zinaachana na vitanda kwa kumuomba Mola wao Mlezi kwa hofu na kutumaini, na hutoa kutokana na tulivyo waruzuku * Nafsi yeyote haijui waliyo fichiwa katika hayo yanayo furahisha macho - ni malipo ya yale waliyo kuwa wakiyatenda**}. Na Mola Mtukufu anasema tena katika wasifu wa wacha-Mungu:

**إِنَّ الْمُتَّقِينَ فِي جَنَّاتٍ وَعُيُونٍ * آخِذِينَ مَا آتَاهُمْ رَبُّهُمْ إِنَّهُمْ كَانُوا قَبْلَ ذَلِكَ مُحْسِنِينَ * كَانُوا قَلِيلًا من اللَّيْلِ مَا يَهْجَعُونَ * وَبِالْأَسْحَارِ هُمْ يَسْتَغْفِرُونَ.**

{**Hakika wacha-Mungu watakuwa katika Mabustani na chemchem * Wanapokea aliyo wapa Mola wao Mlezi. Kwa hakika hao walikuwa kabla ya haya wakifanya mema * Walikuwa wakilala kidogo tu usiku * Na kabla ya alfajiri wakiomba msamaha**}. Na Mtume wetu SAW anasema: "*Ni juu yenu kusimama usiku kufanya ibada kwani ni mwenendo wa waja wema waliokuwepo kabla yenu, na ni kujiweka karibu na Mwenyezi Mungu, na kunakataza kufanya dhambi, kunapelekea usamehevu wa makosa na kunaondoa magonjwa mwilini*".

Ikiwa Ramadhani ni mwezi wa kuachwa huru kutokana na moto, na kila siku ndani ya Ramadhani Mwenyezi Mungu huacha huru waja na adhabu ya moto, basi jambo hilo linategemewa zaidi ndani ya kumi la mwisho, ikiwa Mola wetu Mtukufu anasamehe kwa waombao msamaha wakati wa kabla ya alfajiri, basi rehma hizi na msamaha huu unategemewa zaidi ndani ya kumi hili la mwisho, kutokana na kupatikana ndani yake usiku uliotukuzwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu zaidi kuliko usiku mwengine wowote, nao si mwengine bali ni usiku wa Lailatul-Qadri, ambapo Mtume SAW anasema: "*Utafuteni usiku wa Lailatul-Qadri ndani ya kumi la mwisho la mwezi wa Ramadhani*".

Na usiku huu mtukufu ni usiku bora Mwenyezi Mungu ameteremsha ndani yake Kitabu chenye cheo kikubwa kwa Mtume mwenye cheo kikubwa kupitia Malaika mwenye nafasi kubwa kwa ajili ya Umma wenye cheo kikubwa, nao ni usiku huteremka msamaha rehma na baraka, ambapo Mwenyezi Mungu anasema:

**إِنَّا أَنْزَلْنَاهُ فِي لَيْلَةِ الْقَدْرِ * وَمَا أَدْرَاكَ مَا لَيْلَةُ الْقَدْرِ * لَيْلَةُ الْقَدْرِ خَيْرٌ مِّنْ أَلْفِ شَهْرٍ * تَنَزَّلُ المَلاَئِكَةُ وَالرُّوحُ فِيهَا بِإِذْنِ رَبِّهِمْ مِنْ كُلِّ أَمْرٍ * سَلاَمٌ هِيَ حَتَّى مَطْلَعِ الفَجْرِ.**

{**Hakika Sisi tumeiteremsha Qurani ndani ya (LaylatulQadri) Usiku wa Cheo Kitukufu * Na nini kitacho kujulisha nini Laylatul Qadri? * Laylatul Qadri ni bora kuliko miezi elfu * Huteremka Malaika na Jibril ndani ya usiku huo kwa idhini ya Mola wao Mlezi na kila jambo * Amani usiku huo mpaka mapambazuko ya alfajiri**}. Na Mtume SAW anasema: "*Mwenye kusimama kufanya ibada ndani ya usiku huu kwa imani na matarajio ya malipo basi husamehewa dhambi zake zilizotangulia*".

tunasisitiza kuwa kulainisha nyoyo na kusuruhisha mambo ni mlango wa kukubalika kwa matendo mema, na tofauti pamoja na mivutano ni njia ya kujikosesha na hasa ndani ya masiku haya bora ambapo Mtume wetu SAW anasema: **فِيهِ لَيْلَةٌ خَيْرٌ مِنْ أَلْفِ شَهْرٍ مَنْ حُرِمَ خَيْرَهَا فَقَدْ حُرِمَ** "*Ndani yake kuna usiku wenye cheo ambao ni usiku bora kuliko miezi elfu, mwenye kukosa kheir zake atakuwa amekosa*".

**HOTUBA YA PILI**.

Namshukuru Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, rehma na amani zimwendee Mtume wa mwisho naye ni Mtume wetu Muhammad SAW pamoja na watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake wote.

Ikiwa milango ya utiif ndani ya masiku haya matakatifu ni mingi na ya aina mbalimbali hivyo akili ni lazima ipangilie vipaombele vyake, hivyo hutanguliza lenye manufaa zaidi kuliko lenye manufaa madogo, hivyo husisitizwa ndani ya masiku haya kutoa zaka ya fitri, na inapendeza kufanya haraka kutoa kabla ya siku ya Eid, kwa kuwapa watu mafakiri na masikini pamoja na mayatima na wenye

kuhitaji, na kuwawezesha kukidhi mahitaji yao kabla kuwafikia Eid, ambapo Mtume SAW anasema: أَغْنُوهُمْ عَنِ الطَّلَبِ فِي هَذَا اليَوْمِ "*Watoshelezeni kuepukana na hali ya kuomba ndani ya siku hii*". Na inafaa kutoa fedha kwenye zaka ya fitri, na pesa ndio zinamanufaa zaidi ndani ya jamii yetu na wakati wetu na huwapa nafasi zaidi ya kuhudumia mahitaji yao.

Kama vile Fiqhi ya vipaombele inapelekea kutoa chakula kwa mafakiri na masikini ikiwa kumuondolea tatizo wenye matatizo ndani yake kuna thawabu nyingi, ambapo Mtume SAW anasema:

**أَحَبُّ النَّاسِ إِلَى اللَّهِ أَنْفَعُهُمْ لِلنَّاسِ، وَأَحَبُّ الْأَعْمَالِ إِلَى اللَّهِ سُرُورٌ تُدْخِلُهُ عَلَى مُسْلِمٍ، أَوْ تَكْشِفُ عَنْهُ كُرْبَةً، أَوْ تَقْضِي عَنْهُ دَيْنًا، أَوْ تَطْرُدُ عَنْهُ جُوعًا.**

"*Mtu mwenye kupendwa zaidi na Mwenyezi Mungu ni yule mnufaishaji zaidi watu, na matendo yanayopendeza zaidi kwa Mwenyezi Mungu ni kumletea furaha Muslimu au kumuondolea tatizo au kumlipia deni lake au kumuondolea njaa*". Na Mtume anasema tena:

**مَن نفَّس عن مؤمنٍ كربةً من كُرَب الدنيا، نفَّس الله عنه كربةً من كُرَب يوم القيامة.**

"*Mwenye kumuondolea Muumin tatizo katika matatizo ya dunia, basi Mwenyezi Mungu atamuondolea tatizo katika matatizo ya siku ya kiyama*".

Ewe Mwenyezi Mungu tukubalie funga yetu na kisimamo chetu cha usiku na uilinde nchi yetu ya Misri pamoja na nchi za ulimwengu wa Kiarabu na Kiislamu.

**Amina**